

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**
DAR ES SALAAM
Namba ya Simu:0738166703
Fax: 255 - 022 – 2460117
e-mail: secretary@psc.go.tz;
Website: www.psc.go.tz



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
6 MTA A WA ALBERT LUTHULI,
KITALU NA. 10,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**RUFAA NA MALALAMIKO YA WATUMISHI WA UMMA YALIYOWASILISHWA
TUME KUTOLEWA UAMUZI**

Baadhi ya Rufaa na Malalamiko mbalimbali yaliyowasilishwa Tume ya Utumishi wa Umma na watumishi wa umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Waajiri na Mamlaka zao za Nidhamu yatatolewa uamuzi na Tume, kwenye Mkutano Namba **1** mwaka wa fedha 2020/2021 unaofanyika kuanzia leo Jumatatu tarehe 21 Septemba, 2020 hadi tarehe 02 Oktoba, 2020, Jijini Dar es Salaam.

Shughuli nyingine zilizopangwa kufanyika wakati wa Mkutano huu ni pamoja na kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari hadi Machi) na Robo ya Nne (Aprili hadi Juni) ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Tume inatekeleza majukumu haya kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298.

Imetolewa na:

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Richard M. Cheyo'.

Richard M. Cheyo
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Tume ya Utumishi wa Umma.

DAR ES SALAAM

21 Septemba, 2020